



Zidisheni sana kukikumbuka kikata ladha" Yaani: Kifo

Imepokelewa kutoka kwa Abuu Huraira -radhi za Allah ziwe juu yake- amesema: Amesema Mtume -rehema na amani ziwe juu yake-: "Zidisheni sana kukikumbuka kikata ladha" Yaani: Kifo.

[Ni nzuri (Hasan)] [Imepokelewa na Tirmidhiy, Nasai na Ibn Majah]

Amehimiza Mtume rehema na amani ziwe juu yake juu ya kukithirisha kukikumbuka kifo ambacho kukikumbuka kwake mtu anakumbuka Akhera, na kunabomoa mapenzi yake ya kupenda ladha za dunia ndani ya moyo wake, na hasa hasa zile za haramu.

<https://www.sunnah.global/hadeeth/sw/show/66232>

النجاة الخيرية
ALNAJAT CHARITY

